**MKATABA WA MATUMIZI WA WASHIRIKI WATOTO**

Mkataba huu wa MATUMIZI WA WASHIRIKI WATOTO (“Mkataba” huu), tarehe ya ufanisi ni ile iliyotolewa hapa chini (“Tarehe ya Ufanisi), imeingizwa kati ya Ahadi Kidigitali (Digital Promise) (“Mfadhili”) na ____________________ mzazi au mlezi wa mtoto mshiriki katika programu ya Kibunifu ya Kujifunza ya Verizon (Verizon Innovative learning) (“Mtoto Mshiriki”, ambaye atachukuliwa kuwa kama “mtumiaji” au “wewe” au “wako”) kwa jumla hujulikana kama “vyama”

**Kwa saini yako, unakili na kukubali yafuatayo:**

**MADHUMUNI**

1. Mshiriki mtoto atapata kifaa na huduma bila malipo ili kuwezesha ushiriki katika programu ya Kibunifu ya Kujifunza ya Verizon (Verizon Innovative Learning). Kifaa hiki na huduma ni msaada kutoka kwa Verizon Wireless na hutolewa kwa mtoto mshiriki na Mfadhili chini ya sheria na masharti ya Mkataba huu. Mkataba huu unaweza kusitishwa wakati wowote na Verizon Wireless kwa sababu yoyote. Masharti ya mkataba huu utakua tendaji kutoka tarehe ya utekelezaji na mzazi/mlezi hadi pale ushiriki wa mtoto mshiriki kwenye programu utakatika.

**VIFAA NA HUDUMA**

2. Kifaa hichi kimetengwa kwa matumizi ya Mshiriki mtoto pekee, kwa ajili ya programu, na haiwezi kuuzwa au kuhamishwa kwa mtu au kikundi kingine. Verizon Wireless itatoa huduma za sauti na/au data ili tu kuwezesha ushiriki katika programu; hata hivyo, iwapo Mshiriki Mtoto atakua na matumizi ya kiwango cha juu zaidi, kupiga simu/ujumbe wa kimataifa akitumia kifaa, kupakua sauti au video isiyokua kwa uhusiano na programu, au kupakua michezo, huduma inaweza kukatizwa, kupunguzwa, au kufutiliwa bila ya taarifa. Tamati ya ushiriki wa Mshirika Mtoto katika utafiti, Verizon Wireless itakatiza huduma hizi kwa kifaa na unakubali kurejesha kifaa kwa Mfadhili.

**UTENDAJI WA TAARIFA ZIHUSIANO NA KIFAA NA HUDUMA.**

3. Taarifa kuhusu matumizi ya kifaa na huduma kwa Mshiriki Mtoto, ikiwa ni pamoja na, lakini haijadhibitiwa kwenye, maelezo ya wakati yeye alitumia, huduma za data au kupiga simu na mpigiwa ni habari za Mfadhili, akiwa kama mteja wa rekodi za kifaa na huduma. Kwa hivyo, maelezo haya yanaweza kupatikana na pia kupeanwa kwa Mfadhili, na vyama ambavyo mfadhili ametoa idhini, ikiwa ni pamoja na VGCCO. Hakuna taarifa au maelezo ya kibinafsi yatapatikana na VGCCO.

**SHIDA NA/ AU UKATIZAJI WA HUDUMA**

4. Ushirikiano wa Cellco d/b/a Verizon Wireless (‘’Verizon Wireless”) au wauzaji na wasambazaji wake hawatakuwa na dhima yoyote kutokana na harasa ya mtumiaji, madai au uharibifu uliosababishwa na chochote , ikiwa ni pamoja uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, maalum, juu ya msukosuko au uharibifu, au kwa mapungufu katika huduma, ikiwa ni pamoja na lakini haijadhibitiwa kwa, vurugu au upungufu wa huduma zilizotolewa kama ilivyoandikwa kwa huu mkataba, bila kufuatillia aina ya hatua, iwe ni kwa mkataba au kwa makosa ya kisheria au vingineyo. Ukomo huu ni pamoja na hasara, uharibifu, madai au gharama za aina yoyote inayotokana na matumizi au kujaribu kutumia huduma, au kukosa uwezo wa kufikia mifumo ya ufuatiliaji wa maisha au vifaa, 911 au E911 au simu nyingine au huduma za dharura. Huwezi kudhaniwa kuwa mrithi wa tatu wa mkataba wowote kati ya Mfadhili na Verizon Wireless.

**USULUHISHI**

5. **MTUMIAJI ANAKUBALI YA KWAMBA, KADIRI YA KIWANGO KAMILI CHA SHERIA:**

(i) MABISHANO YOYOTE AU MADAI YANAYOCHIPUKA NJE YA AU KATIKA MKATABA HUU, AU KWA KIFAA AU HUDUMA INAYOPEYANWA CHINI AU KWA UHUSIANO NA HUU MKATABA, ITATEKELEZWA NA USULUHISHI HURU UTAKAO JUMUISHA USULUHISHO USIOTEGEMEA UPANDE WOWOTE NA KUTEKELEZWA NA AMERICAN ARBITRATION ASSOCIATION ("AAA") CHINI YA SHERIA ZA WIRELESS INDUSTRY ARBITRATION ("WIA"), KAMA ZILIVYOREKEBISHWA NA HUU MKATABA. MAELEZO YA SHERIA NA MALIPO YA WIA YANAPATIKANA KATIKA www.adr.org. **USULUHISHI SIO MOJA WAPO YA MAENDELEZO YA MAHAKAMA. KANUNI ZA USULUHISHO NI TOFAUTI NA KANUNI ZA MAHAKAMA. HAKUNA JAJI AU BARAZA LA WAAMUZI KATIKA MAENDELEZO YA USULUHISHO.** KIFUNGU HIKI CHA USULUHISHO KITATUMIKA KWA MADAI YOTE AMBAYO MTUMIAJI ANAWEZA KUDAI DHIDI YA MFADHILI AU VERIZON WIRELESS NA KWA MADAI YOYOTE AMBAYO MFADHILI AU VERIZON WIRELESS WANADAI DHIDI YA MTUMIAJI. VERIZON WIRELESS NI MFADHILI AKIWA KAMA MUHUSIKA WA TATU KWA TAARIFA YA MKATABA HUU.

(ii) Sheria ya Federal Arbitration inatumika kwa mkatamba huu. **IWAPO SHERIA INAYOTUMIKA ITARUHUSU UWAKILISHWAJI AU SULUHISHO KWA UWAKILISHWAJI, MTUMIAJI HANAHAKI YOYOTE YA KUZINGATIA USAIDI WA KESI AU MADAI DHIDI YA MFADHILI AU VERIZON WIRELESS, AU WASAIDIZI AU WAFUASI WAO.** Iwapo madai mengi yameunganishwa katika hatua moja, na baadhi hayatazingatia usuluhishi, madai hayo ya mwisho yanapaswa kuachwa mpaka madai yoyote katika hatua hiyo ambayo yanakubaliwa na usuluhishi yametatuliwa. Ikiwa kuna madai dhidi ya vyama vingi, ambapo baadhi yao hawakutakikana kwenye usuluhishi, madai kwenye usuluhishi lazima yatengwe; Hata hivyo, mtumiaji anadumisha haki yake ya malalamiko kwa idara au tume ya udhibiti.

(iii) Hakuna msuluhishi mwenye mamlaka ya kupeana misaada zaidi ya kile mkataba huu umeruhusu, au kuagiza mipango au kesi za usuluhishi, isipokuwa pale msuluhishi ameamua kuwa madai yanayochipuka au kuhusiana na maakubaliano ya awali yanaweza kutoa msaada mkubwa kwa muktadha usio wa kesi kwa msingi wa makubaliano ya awali. Katika usuluhishi wote, msuluhishi lazima awe na athari kwenye sheria zinazohusika na makataa na itatumika kuamua iwapo suala litahusisha msuluhishi au la. Katika usuluhishi Mkubwa/wa Kukanganya, wasuluhishi wanapaswa pia kutumia Kanuni za Federal Rules of Evidence na mhusika anayepoteza anaweza kuamulu tuzo kukaguliwa na jopo la mapitio lililo na wasulihishi (3) watatu

| **Mzazi au Mlezi (Mshiriki Mtoto):** | **Ahadi Kidigitali (Digital Promise) (Mfadhili):** |
|---|---|
| Saini Hapa: | Saini Hapa: |
| Jina la Chapa: | Jina la Chapa: |
| Anwani: | Anwani: |
| Tarehe: | Tarehe: |
| Jina la Mshiriki Mtoto: | |

**Tafadhali jaza kila mstari hapa chini ili kudhibitisha unaelewa na unakukubali:**

| **Neno** | |
|---|---|
| | Ninaelewa kwamba ninahitaji kufuatilia matumizi yangu ya data ili isizidi kiwango cha 5GB kwa kila mwezi na sifai kupakua sauti au video isipokuwa pale kuna uhusiano na programu, na siwezi kupakua michezo. |
| | Nakubali kutopakua programu za kulipwa au zilizolipiwa (programu) |
| | Nakubali kutotumia vipengele vingine vyovyote vya kifaa  ambavyo havihusishwi na programu ( yaani, Hotspot Binafsi, nenosiri la SIM) |
| | Nakubali kutoondoa sehemu yoyoteya kifaa (yaani chipu ya SIM) au programu ya kifaa isipokuwa kwa idhini ya Verizon Wireless |
| | Nakubali kutumia kifaa nilichotengewa tu ndani ya majimbo 50 ya Marekani. |
| | Nakubali kutopiga simu au kuandika ujumbe wa kimataifa, video au picha, ikiwa ni pamoja na simu na ujumbe kwa nchi za Canada na Mexico |
| | Ikiwa kifaa nilichopewa kimepotea au kuibiwa, ninakubali kuripoti mara moja kwa: Ahadi Kidigitali (Digital Promise), Michael Mades |
| | Ninaelewa kuwa ikiwa kifaa changu hakitumiki kutokana na kasoro ya mtengenezaji, ninaweza pokea nafasi moja ya udhamini, kwa hiari ya VGCCO au Verizon. Ninaelewa kwamba ikiwa nitapata kifaa mbadala na, kikapotea au kikaibiwa au kikaharibika, ikiwa ni pamoja na skrini iliyovunjika, hakitabadilishwa na nitaondolewa kwenye programu |

| | |
|---|---|
| | Ninaelewa kwamba kifaa ni kwa matumizi yangu tu, ili kuwezesha ushiriki katika programu, kwamba siwezi kuuza au kupeana kifaa kwa muhusika yeyote wa tatu au kuruhusu mtu yeyote kutumia huduma kwa madhumuni mengine yasiyokuwa na uhusiano na programu. |
| | Ninaelewa kwamba kifaa ni matumizi yangu tu, ili kuwezesha ushiriki katika programu, kwamba siwezi kuuza au kupeana kifaa kwa muhusika wowote wa tatu au kuruhusu mtu yeyote kutumia huduma kwa madhumuni mengine isipokuwa na uhusiano na programu. |
| | Ninaelewa kuwa Verizon Wireless au VGCCO inaweza kusimamisha au kusitisha huduma wakati wowote, bila ya taarifa. |

Ninaelewa kwamba nikikiuka mojawapo ya sheria hizi, nitapata kuondolewa kutoka kwa programu na lazima nirejeshe kifaa changu kwa meneja wa programu ya Kibunifu ya Kujifunza ya Verizon (Verizon Innovative Learning).

_______________________________________________ ____________________________________

Mtumiaji Tarehe